



Mapendekezo ya kutumia mbolea katika kilimo cha muhogo Tanzania

Chapisho la Ekari



HATUA 1: Mbinu bora za kilimo

HATUA 2: Kuchagua mbolea sahihi

HATUA 3: kiwango kinachostahili cha mbolea

HATUA 4: Kokotoa gharama za uzalishaji na faida

HATUA 5: Kuweka mbolea kwa wakati

HATUA 6: Njia ya uwekaji mbolea

HATUA 1: Kutumia Mbinu Bora za Kilimo

Mbolea inashauriwa itumike ikiwa mbinu mbora za kilimo zimefuatwa:

- Kila mara tumia mbegu bora zinazohimili magonjwa mfano Mkombozi, Mkuranga 1 au Kiroba. Tembelea tovuti <https://seedtracker.org/cassava/>
- Tunashauri kupanda mbegu zilizothibitshwa na zisizo na magonjwa.
- Pand kwa nafasi ya mita moja (m1) kati ya mstari na mstari, na mita moja (m1) kati ya shina na shina (mimea 4,000 kwa ekari).
- Andaa shamba vizuri ili kudhibiti magugu. Angalia Mapendekezo kwenye kipeperushi cha "Kanuni za Msingi za Kilimo cha Muhogo Tanzania".

HATUA 2: Chagua Mbolea Sahihi

Muhogo unahitaji virutubisho mbalimbali kukua. Virutubisho 3 ambavyo ni muhimu zaidi ni:



Nitrojeni inahitajika kwa ukuaji wa shina na majani.



Fosiforasi Huupa mmea nguvu ambayo husaidia mmea katika ukuaji



Potasiamu huhitajika kutengeneza mizizi yenye afya

Baadhi ya mbolea zinavyo virutubisho vyote vitatu (m.f. NPK 15:15:15, NPK 17:17:17 au NPK 20:10:10) wakati mbolea nyingine zinavyo virutubisho 1 au 2 tu (m.f. urea 46:0:0, DAP 18:46:0 na MOP 0:0:60).

Muhogo unahitaji virutubisho vyote 3 ila kiwango kinategemea na rutuba ya udongo na muda wa kupanda. Kwasababu hii inafaa kutumia mchanganyiko wa mbolea tofauti kuliko kutumia mbolea moja yenye virutubisho vingi. **Katika nyezo hii tutaangazia matumizi ya mbolea zinazopatikana Urea, DAP and NPK 17:17:17.**

HATUA 3: Weka kiasi cha Mbolea Kinachostahili

Kiasi cha mbolea cha kuweka kinategemea mavuno yako ya sasa. Fikiri jinsi muhogo ulivyostawi katika shamba lako, na ulinganishe saizi ya mihogo kwenye shina na picha.



CHINI

Chini ya tani 3 kwa ekari



KAWAIDA

Tani 3 - 6 kwa ekari



WASTANI

Tani 6 - 9 kwa ekari



MENGI

Tani 9 - 12 kwa ekari



MENGI SANA

Zaidi ya tani 12 kwa ekari

Ikiwa mavuno yako ya sasa ni mengi, ndivyo mbolea inavyohitajika kidogo. Tumia kipeperushi chenye ramani ili kupata kiasi cha mbolea kinachopendekezwa katika wilaya yako. Mapendekezo hutolewa kwa kilo ya mbolea mfano Urea, DAP, na NPK kwa ekari. Badili kiasi hichi kulingana na ukubwa wa shamba.

Eneo la shamba lako (ekari) x Kiasi cha mbole kinachohitajika (kg)

=

Kiasi cha mbolea kinachohitajika kwenye shamba lako (Kg)

Mfuko 1 (wa 50kg) kwa ekari ni sawa na vifuniko 2 vya chupa ya Maji kwa muhogo



HATUA 4: Kokotoa Gharama na Faida

Matumizi ya mbolea yatakua na maana Endapo mavuno yatakua mengi zaidi ya gharama ya mbolea. Kiasi kinachopendekezwa kinakokotolewa kwa kutumia bei ya mihogo na bei ya mbolea katika eneo lako.

Inakulazimu kuhakikisha faida kwenye matumizi ya mbolea. Kokotoa gharama na faida inayotarajiwa.

Ongezeko la Thamani Linalotarajiwa

$$\text{Bei ya tani 1 ya muhogo (TZS)} \times \text{Mavuno ziada yanayo tarajiwa (tani/ekari)}$$


*Muza Pembejeo anaaminika anaweza kukupa bei ya mbolea

Jumla ya Gharama ya Mbolea

$\frac{\text{Bei ya mfuko 1 wa Urea (TZS)}}{\text{Uzito wa mfuko 1 wa urea (kg)}} \times$	Urea inayohitajika kwa ekari 1 (kg)
$+$ $\frac{\text{Bei ya mfuko 1 wa DAP (TZS)}}{\text{Uzito wa mfuko 1 wa DAP (kg)}} \times$	DAP inayohitajika kwa ekari 1 (kg)
$+$ $\frac{\text{Bei ya mfuko 1 wa NPK (TZS)}}{\text{Uzito wa mfuko 1 wa NPK (kg)}} \times$	NPK inayohitajika kwa ekari 1 (kg)

Urea, DAP and NPK 17:17:17 inayohitajika kwa ekari 1, na ongezeko la uzalishaji linalotarajiwa hupatikana kwenye vipeperushi na ramani.

Tuangalie uwezo wako katika kukubali changamoto. Unaweza mara ngapi katika bidhaa au teknolojia mpya za kilimo?



HATUA 5: Kuweka Mbolea kwa Wakati Muafaka

- Weka mbolea kwenye udongo wenye unyevu, baada ya mvua kunyesha
- Weka kipimo kamili cha DAP wakati wa kupanda.
- Urea na NPK 17:17:17 ni vizuri ziwekwe kwa kugawanywa mara 2 hadi 4 katika kipimo sawa. Weka mbolea ya kwanza mwezi 1 baada ya kupanda. Kisha weka vipimo vinavyofuata kwa jinsi mvua itakavyoruhusu, baada ya miezi 2 hadi 3. Weka NPK wakati wa mgawanyo wa 1-2, na baadae Urea.

HATUA 6: Weka Mbolea kwa Usahihi

- Chimba mtaro wa duara au nusu duara wenye kina cha sm 5 na umbali wa sm 20 kutoka kwenye shina la muhogo
- Weka kiasi kinachohitajika cha mbolea kwenye mtaro na fukia
- Uwekaji wa kiasi sawa cha mbolea kwenye kila shina la muhogo ni mgumu na unahitaji mazoezi. Kutumia mfuniko wa chupa ya maji kunasaidia kupata kiasi sahihi (Angalia ukurasa wa mbele).



Kwa watumiaji wa Vodacom Tanzania wanaweza kupata taarifa hii kwa kupiga namba 321

WASILIANA NA: akilimo@cgiar.org
au tembelea tovuti ya www.akilimo.org

